# NYUMBA ZA WALIOKOKA KIBIBLIA

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha NYUMBA ZA WALIOKOKA KIBIBLIA. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

NYUMBA ZA WALIOKOKA  KIBIBLIA

1.Mafanikio uliyonayo……………………………………………….

2. Mwili wako………………………………………………………….

3. Mapango wa mungu ktk nyumba yako……………….…

4. Mambo ya kuzingatia ……………………………………...

5. Maombi ya kuweka nyumba wakfu……………………

6.Shukrani…………………………………………………………

7.Kuokoka…………………………………………………………

8. Mwisho…………………………………………………………

# 1. MAFANIKIO ULIYONAYO

Mafanikio uliyonayo kabla hujaokoka mtu wa kimaitaifa mfano lubani ktk shirika la ndege la kimaitaifa uliyapata ukiwa mbali na mungu ni mwenye dhambi pengine kwa njia dhambi kwa rushwa au kuuza kasino au bar, kwa kuiba pengine kutumia nguvu za giza ktk kupata hiyo kazi au ktk biashara na njia zinginezo mbaya/mbovu. Hivyo mungu anayachukia hayo maasi aliyokutwaa umeokoka utende tena umeamua kurudia mungu tosheka kile unachoa pata kwa haki

Hayo ni mafanio uliyopata nje ya mungu una mali hoteli, Kampuni,Pesa,Nyumba,Samani, mavazi,viwanja n.k ukiwa mwenye dhambiJehesabu mbele za mungu kama huna kitu ndio kwanza kutafata mbele za mungu mafanio kama hayo mara dufu na kupita.

Unatakiwa kupata mafanikio mapya ndani ya Yesu hayo ndio yanayompendeza mungu uwe hodari kwa haki. Mafanikio hayo huitwa baraka au utajiri wa mungu maana utapata kwa nguvu za mungu. Mafanikio nje ya mungu ukiwa mwenye dhambi na mafanikio ndani ya Mungu Kwa kumtii.

Na upate ufahamu kidogo juu ya kupata mafanikio yaani utajiri au baraka ktk shughuli ya kazi ya mikono yako ktk kanisa lolote la waliookoka.

- Unatakiwa kuchangia injili yaani mikutano ya injili.
- Toa fungu la kumi au zaka.
- Changia ujenzi wa jengo la kanisa ikitokea
- Changia sadaka zote zilizaomriwa kanisani.
- Mkumbushe mungu ktk maombi yako ktk chumba ndani ya nyumba yako walau hata masaa matatu juu kile ulichochangia ktk  kazi kama ni injili mwambie akuletee wateja wa faida unayotaka kwa siku,week au mwezi wa kutosha ile unacho cha kumtolea kwa kazi yake ktk biashara yako au kampuni unayomiliki.

## 2.MAFANIKIO ULIYONAYO

- Mwombe Mungu ukupe Baraka au utajiri ktk kazi za mikono yako kwa ajili ya kuchangia kazi yake kama injili.
- Uwe mtu wa shukrani kwa baraka au utajiri anakupa mungu yaani baba yake Yesu kwa kumwambia asante mf. Kwa kuniwesha kufungua kampuni nyingine ktk maombi yako au kumtolea sadaka ya kumshukuru kwa mfano wa jambo kama hilo.
- Ikiwa unatenda hayo ktk kanisa la waliokoka kwa zaidi ya miaka 3 na Mungu hajakupa baraka au utajiri, mungu hajakuinua umebakia na yale mafanikio ya dhambi na mapato yako yamepungua kwa sababu uliacha ukaanza maisha mapya kwa kumtoea miaka hiyo yote hujafungua chochote tafuta ushauri kwa mtumishi wa kanisa ukautumia ikishindikana jitahindi kutafuta kukutana na mtumishi mkuu wa kanisa au huduma imeshindikana nawe huwezi kuvumilia hiyo hali tafuta kanisa au huduma nyingine ya waliokoka unayoamini ukishirikiana nao utainuliwa.

Kabla ya kuokoka ulikuwa na manifanikio pengine ya dhambi kwa rushwa, kuiba kazini, uongo au dhuluma baada ya kuokoka njia za dhambi za kupata pesa unaziacha unabaki na za haki matokeo yake kipato chako kimepungua unachopata kwa siku au kwa mwezi mshukuru mungu kwa hilo karibu ktk wokovu yapo mambo mazuri ukiweza kumtii mungu. Hayo usiyahesabu kuwa yalitoka kwa mungu bali utakayopata kupitia utoaji na kuweza vitu vya haki ndiyo yanayotoka kwa mungu.

Mfano: kabla ya kuokoka ulikuwa na kampuni saba kati ya hizo nne ulizipata kwa rushwa,dhuluma na kuuza madawa ya kulevya ni kampuni za vitu vya dhambi mfano pombe au sigara hivyo unapooka unatakiwa kufunga viwanda vyako vinne na kubaki na vitatu. Sasa vile viwanda vitatu unavyoendesha ukipata faida zake kila wiki au wezi unachangia kazi ya mungu ukifungua kiwanda cha nne cha haki

# 3. MAFANIKIO ULIYONAYO

Hicho ndiyo baraka ya kwanza kutoka kwa mungu pengine baada miaka 3  umefanikiwa hivyo kutokana na utii wako kwa mungu wa kuchangia kazi ya mungu kama injili na zaka au fungu la mungu. Yesu aliahidi kwa mtu anayepoteza mali yake kwa ajili ya kumfuata ktk dunia hii kumlipa mara mia ikiwa hapa duniani na uzima wa milee.

Mfano huu una maana ulipoteza vinne unatakiwa kuvitafuta mbele za mungu naye atakupa na kuzidi uwe hodari na mwaminifu ktk matoleo ili akufanikishe kukurjeshea ulivyopoteza na kuzidi,Pengine kwa utoaji mungu anakujalia kila baada ya miaka 2 unafungua kampuni na kufanya vizuri ndani ya miaka 12 unakuta umefungua 6 kampuni za vitu vya haki kama nguo,mikanda au kiatu zinazofanya vizuri na ile 1 uliyoipa kwa matoleo mbali na zile 3 toka uokoke unakuwa na kampuni 7. ukichukua na zile 3 kabla hujaokoka na 7 baada ya kuokoka jumla 10. Baraka ya mungu zile 7 ulizokupa ktk

Ukitaka utajiri wa Yesu tafuta zifike mia. Yotekwa ajili ya injili ya Yesu mungu akuita ulale huku amekuita ukeshe ktk maombi usiku na kuomba utajiri au baraka ya kwa ajili ili akuongeze kimawazo na kukupasha habari ni kitu gani ukiwekeza utakipata kwa wingi.

Usianzishe kitu cha haki bila kumshirikiasha mungu kwanza ulizoea kabla hujaokoka kwenda kwa watu na kuwashirikisha kama unataka kufungua biashara au kampuni lakini

# 4. MWILI WAKO

Ufahamu mwili wako kabla kuokoka mwili wako uliku-wa nyumba ya dhambi ila baada ya kuokoka mwili wako ni nyumba ya mungu na Hekalu la Roho mtakatifu Msaidizi wetu ktk mambo ya Yesu.

Kutunza mwili wako baada kuokoka kama nyumba yangu na mungu na Hekalu la roho mtakatifu usifanye dhambi hasa za asili ya zinaa kama uasherati,uzinzi au ufiraji asije mungu akukuharibu maana anaishi ndani yao huo mwili ukaona maisha ya wokovu magumu kupi-ta yale kabla hujaokoka hivyo ukalaani maamuzi yako ya kuokoka.

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka wewe ni mtu mwenye elimu ya hekima ya kibadamu wala si ya mungu ufahamu neno hili ili kushinda zinaa uasherati,ufiraji au uzinzi lazima uizidi haki ya farisayo aliyekuwa anafunga mara mbili kwa juma. Hilo moja Epuka kutumia vyakula vya protini.Kama kijana umeokoka na umebarehe na umepevuka jjifunze kufunga zaidi ya mara mbili kwa ju-ma na kupueka matumizi ya vyakula vya protini (Yazimishe mapenzi ndani yako uwe kama mtoto). Ichunguze tamaa ya mwili imefikia kama kabla hujab-arehe au kupevuka ulipokuwa mtoto dumu na hicho ki-wango cha kitoto ukijianda kwa kuoa na kujishughul-isha. Uwe kama yule mtotio uchanga asiye na mawazo ya upendo kwa mwanamke au mwanaume ukiwa neno la imani alilosema mungu zaeni mkaongezeke jiandae kwa kuoa au kuolewa. Utashinda kwa kufunga na kujiepusha vyakula protini na marifiki wa zinaa kama wazinzi, wafiraji,washerati, Malaya au makahaba.

## 5. MWILI WAKO

Ila kama umeoa au umeolewa upo ktk ndoa ujue upo ktk majumu ya kutafuta baraka ya mtoto au watoto kutoka Mungu aliyeukuumba kumshirikisha mungu kwa maombi hata wewe na mkeo kimaelezo ya kidaktari hamna tatizo na pengine umezaa wawili unafuta watatu ili usije ukazaa mtoto mwenye kasoro za uumbaji asiyefanana na Yesu kimwili akizaliwa dunia anayemkubali Mungu na Yesu na kuokoka asiyemkataa Mungu na Yesu hata kuokoka akizaliwa si mtoto wa kwenda jehanamu. Kwa walioa kuizidi ya ya Farisayo ya kufunga mara mbili kujuma ni ya lazima kutumia vyakula vya protini kwa kiasi ili kukabili jukumu la ndoa ni muhimu

Ikiwa kabla kuokoka hupitishi mwaka,miezi,wiki au siku tatu bila kufanya uzinzi au uasherati uzinzi jifunze kuuzoeza mwili kwa mfungo na kuepuka matumizi ya vyakula vya protini mpaka mwili wako utakapogeuzwa kama mtoto mchanga asifanye dhambi za zinaa kama uzinzi. Kujiepusha na wazinzi na kuombe mungu asikutie ktk vishawishi vya uzinzi ni muhimu.

Hizo ndio njia za kuepuka zinaa dhambi ambayo Yesu anaichukia nduguye kutokuamini:=>

=>Kufunga zaidi ya siku mbili ktk juma

=>Kuomba uepushwe na vishawishi vya zinaa

=>Kuepuka matumizi ya vyakula protini kama mayai

=>Kujiepusha na marafiki wa kale wazinzi au washerati

=>kujiepusha na vitu vinavyochochea mapenzi kama vitabu/picha/tamthilia  za mapenzi, picha za ngono n.k

## 6. MPANGO WA MUNGU KTK NYUMBA YAKO

Nyumba niliyokuhubiri yaani mwili ni mambo ya kiroho usimjaribu mungu kwa maana anaishi ndani yako na Yesu kwa njia huyo msaidizi yaani roho mtakatifu. Mpango wa mungu kwa mwili wako ni kuutumia mwili wa kufanya mapenzi yake kama kuhubiri,kuuzoeza maisha ya haki, kumwabudu, kutenda ishara kama kutoa, pepo,kuponya au miujiza au kubariki wengine.

Lakini huo mwili ambao ni nyumba ya mungu na hekalu la roho mtakatifu unaitaji malazi kwa kulaza kichwa yaani nyumba zinazojengwa na mafundi washi ktk dunia.

Kama uliyeokoka ee mtu wa kimataifa mpango wa mungu ktk nyumba unayojenga anataka aone mahitaji yake yanajumuishwa ktk kujenga nyumba yako mbali na mahitaji yako baada ya kupata baraka au utajiri wa Mungu kwa kuchangia kazi za mungu kama injili.

=> Chumba cha ndani cha kusali au maombi

=>Chumba cha wageni.

Haya ni mambo mawili ya muhimu kuhusu nyumba ya aliyeokoka yaliyo ktk injili yenye kufaidia wokovu wako.Kuwa na chumba maombi mpango wa mungu upeleke mahitaji yako kumwabudu na kumwabudu mungu kila siku usiku wewe na familia yako na kuwa na chumba cha wageni usikose baraka ya mungu kupitia mgeni anayekutembelea hii itawezekana sana kama unatabia kuomba kutembelewa na mgeni mwenye baraka zako.

Ukweli ulipookoka ulipewa uwezo wa kufanana na mungu. Nyumba mungu ni wewe na ile ya kutengenezwa na

## 7. MPANGO WA MUNGU KTK NYUMBA YAKO

Waashi ambalo ni hekalu kazi za mikono ya wanadamu. Kumbuka mwili wako ni hekalu la roho mtakatifu na wewe u kazi ya mungu. Maana ya hekalu ni nyumba ya mungu hivyo mungu ktk dunia ana mahekalu mawili la kwanza mwili wako na la pili ni lile la kujengwa waashi.

Tumemaliza kuzungumzia mwili kama hekalu na-zungumzia hekalu la kujengwa na waashi. Ikiwa umepewa uwezo wa kufanana na mungu  na mungu aliamuaru waisraeli hapo zamani wamjengee hekalu ili akae nao ka-ma malazi yake wew ukitaka kufanana naye kwa malazi ya mwili jenga nyumba ya kufanana na hekalu siyo hekalu ambayo ni ghorofa ya orofa mbili au ghorofa ya orofa sita. Huo ndio mpango wa mungu kwako ikiwa unata kufanana ktk vipimo urefu 27m kwa upana 9m kwa kimo 13.5m kwenda juu (**1wafalme 6**) au  up 50m na up 50m na kimo 40 m kwenda juu(**Nabii Ezikiel 40-44).** Mfano unatakiwa kununua kiwanja cha urefu wa  30m kwa upana wa 15m (Mfalme) au  up 60m kwa up 60 (**Nabii Ezikiel 40-44**).

Kwa maana nyingine unatakiwa kujenga malazi ya kufanana na mwili wako ambao ni hekalu la Roho mtakati-fu na nyumba ya mungu. Nyumba yako ya kujenga kwa kutumia waashi narudia ni ghorofa ya orofa mbili au sita bila kusahau kuweka chumba cha maombi na cha wageni usifikiri sebule ni chumba cha ibada ila ulijikuta umeokoka na pengine unatumia sebule kwa ibada, kula hata kupumzisha akili ulijenga ukiwa hujaokoka na hujui kweli.Ukipata baraka ya kwanza kujenga nyumba yako mpya baada ya kuokoka ee mtu wa kimataifaifa zingatia hayo. Chumba cha maombi ni muhimu kuomba mahataji yako mbele za mungu malengo,familia na shughuli zako

8. MAMBO YA KUZINGATIA

Yesu alisema ni nani? Atakaye kujenga nyumba asikaa chini na kuhesabu gharama asije akajenga akashindwa kumaliza watu wapitao njiani wakaiona na kumcheka.

Unapotaka kujenga nyumba yako zingatia mambo yafutayo:

⇒ Orodhesha mahitaji yako mfano chumba cha kulala,jiko,sebule,choo n.k

⇒ Jumuisha na mahitaji ya mungu yaani chumba cha ndani na cha wageni.

⇒ Gharama ya nyumba unayotaka kujenga mfano ya Tshs.70 milioni au ni Tshs 100 milioni. Mtu wa kimataifa uliyeokoka unatakiwa kujenga ghorofa ya orofa mbili au sita inayofanana na hekalu. Jifunze kuuliza gharama kwa waashi au kampuni za ujenzi wa nyumba.

⇒ Hata kama unapesa ya kujenga ghorofa yote penda kupatana na mwashi au kampuni ya ujenzi na uoneshe ramani yako kwa orofa moja baada nyingine kwa malipo.

⇒ Ukianza lile jengo la chini hakikisha linaisha na unaweka kila kitu kama rangi,umeme,madirisha,milango,marumaru ,feni gymsum na zege la kufunika paa kabla ya kuweka orofa ya juu ili usije Chekwa pesa ikikata njiani. Lile jengo la chini likiisha unakuwa na uwezo hata ya kuhamia.

⇒ Ikiwa Pesa inaruhusu ndipo unaendelea na ujenzi wa orofa ya juu ya jengo la chini likiisha lote unaangalia pesa ulionayo inaruhusu kuendelea na ya tatu unafanya hivyo kwa kila orofa unayojenga mpaka unamaliza ghorofa lako pesa ikata njiani unakuwa uchekwi.

## 9. MAOMBI YA KUIWEKA WAKFU NYUMBA YAKO

Ukimaliza nyumba yako au ghorofa kwa mtu uliyeokoka kama wewe mtu wa kimataifa uliyeokoka kabla ya  kuhamia iweke wakfu kwa kumwita mtumishi wa mungu au mchungaji akaiombea/kufanya ibada kwa ajili ya kuiweka nyumba au ghorofa yako  wakfu kwa mungu.

Unaikabidhi nyumba au ghorofa yako kwa mungu kupitia hayo maombi. Hivyo ndivyo utakavyofanya mali zako zote uzipatazo kwa mungu ili kuzifanya kuwa za mungu na mungu ana uhalali wa kuzitumia mfano gari,kampuni,kiwanja n.k

Mali yako unatakiwa kuiona ni ya mungu ili mungu ikiitaka kwa kazi yake kama ile ya injili usijisikie shida moyoni kumpa mungu. Yesu alisema hamuwezi kumtumikia mungu na mali. Uliyeokoka wewe umechagua kumtumikia mungu jifunze hata mali yako kuitumia kwa kumtumikia mungu kwa kuchangia kazi yake kama ujenzi wa jingo la kanisa.Uwe tofauti na mwenye dhambi aliyechagua kuitumikia mali badala ya mungu mali yake haitumii kwa kuchangia kazi ya mungu bali kwa shughuli zingine na kustarehe.

**Walawi 27:14**

**"Na mtu atakapoiweka nyumba yake iwe <u>wakfu</u> kwa Bwana ndipo kuhani ataihesabu kima chake hiyo nyumba, ikiwa njema ikiwa mbaya; kama kuhani atakavyoihesabu kima chake ndivyo itakavyokuwa. "**

**Walawi 27:14**

**"Tena kama mtu akiweka wakfu kwa Bwana sehemu ya shamba la milki yake, ndipo hesabu yako itakuwa kama kule kupanda kwake kulivyo; kupanda kwake homeri moja ya mbegu ya shayiri, kutahesabiwa kuwa ni shekeli hamsini za fedha. "**

Kuweka kitu wakfu ni kufanya hicho kitu kuwa mali mungu au cha mungu.vitu vyote vyako ukivitoa wakfu vinahesabika ni vya mungu.

## 10. SHUKRANI

Mshukuru Mungu kwa kukuwezesha kumaliza kujenga ghorofa ya maombi na kwa kumtolea sadaka ya shukrani kanisani unakoabudu mungu. Jifunze kushuru kwa baraka au utajiri akupao baba yake Yesu kwa ajili ya injili ya mwanae Yesu kama fedha/pesa,watoto,afya,chakula,kampuni viwanja,biashara n.k

### Walawi 7:12

**"Kwamba aitoa kwa ajili ya shukrani, ndipo atakaposongeza pamoja na hiyo sadaka ya shukrani mikate isiyotiwa chachu, iliyoandaliwa na mafuta, na mikate ya kaki isiyochachwa iliyopakwa mafuta, na mikate ya unga mwembamba uliolowama mafuta. "**

Walawi 19: 23 –24

**"Nanyi hapo mtakapoingia nchi ile, mkiwa mmepanda miti ya namna zote kwa ajili ya chakula, ndipo mtayahesabu matunda yake kama ni kutotahiriwa; muda wa miaka mitatu miti hiyo itakuwa kwenu kama kutotahiriwa; matunda yake hayataliwa.**

**Lakini mwaka wa nne matunda yake yote yatakuwa ni matakatifu, kwa ajili ya kumpa Bwana shukrani. "**

2 kor 1:11

**"ninyi nanyi mkisaidiana nasi kwa ajili yetu katika kuomba, ili, kwa sababu ya ile karama tupewayo sisi kwa msaada wa watu wengi, watu wengi watoe shukrani kwa ajili yetu. "**

Kwa maandiko hayo juu mungu hupendezwa na shukrani. Mungu humfanikisha na kumtendea zaidi mema yake mtu mwenye moyo wa shukrani . Kumwambia mungu asante kwa maneno ya kinywa chako au sadaka yako kunampendeza Mungu yaani Baba yake Yesu.

## 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**


Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :

**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 35666

Mwenge DSM Tanzania



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034